**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**

**SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**SHULE YA SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA**

**S.L.P 145**
**KILOSA**

**Mkuu wa Shule: 0754393921** **Tarehe 24/04/2025**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0656140560**

**Matron: 0658681558**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………….**

**S.L.P ……………………………………..**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA ILIYOPO**

**HALMASHAURI YA KILOSA MKOA MOROGORO MWAKA WA MASOMO 2025/2026**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025/2026 na atasoma tahasusi aliyopangiwa na serikali

Shule ya Sekondari ya Kilimo Kilosa ipo umbali wa Kilometa 28 Mashariki mwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa au kilometa 47 Magharibi mwa mji wa Dumila. Kuna njia mbili za usafiri zitakazo kufikisha shule ya Sekondari ya Kilimo Kilosa.

Mosi, **usafiri wa gari moshi (treni ya kati na mwendo kasi).** Tunawashauri watakao amua kutumia njia hii kutoka Dar es salaam, Morogoro, Dodoma, Kigoma na mikoa ya kanda ya ziwa. Nenda stendi ya mabasi ya wilaya ya Kilosa, Panda gari zinazokwenda Dumila. Shuka kituo cha Rudewa (nauli ni tsh 3000 tu). Chukua bodaboda wakulete Kilosa sekondari (kizunguzi) na nauli ya bodaboda ni Tsh **2000** tu.

Pili, **usafiri wa mabasi** kwa watakaotumia njia inayopitia mkoa wa **DODOMA** washuke kituo cha Dumila. Ulizia stendi ya magari yanayo kwenda kilosa, Panda gari hiyo inayokwenda kilosa halafu shuka kituo cha Rudewa (**nauli ni Tsh 4,000/=**). Chukua bodaboda hadi shuleni. Kwa watakao tumia njia inayo pitia Chalinze (Pwani) na mkoa wa Iringa, shuka kituo cha mabasi cha mkoa wa Morogoro (MSAMVU). Panda gari ya kilosa kupitia **Dumila** na shuka kituo cha Rudewa **(Nauli ni Tsh 8,000)**, panda bodaboda hadi shule.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **08/07/2025** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **06/07/2025** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **14/07/2025**

Ni vizuri mtoto wako akafika siku iliyopangwa ya kufungua shule ili tarehe **08/07/2025** awe darasani anasoma.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Aje na Suruali mbili za rangi ya damu ya mzee (Redish Brown) iwe na marinda mawili kulia na mawili kushoto isiwe ya kubana yaani "Model" upana chini usipungue sentimeta 16. (inapatikana eneo karibu na shule kwa gharama ya tsh 20,000 kwa kila suruali)

ii. Mashati mawili au zaidi meupe ya mikono mifupi yasiyo bana au pwaya sana mwili **(yanapatikana eneo karibu na shule kwa gharama ya tsh 15,000 kwa kila shati)**

iii. Sare za michezo ni jezi ya rangi ya blue kwa wanaosoma tahasusi ya HKL na jezi ya rangi nyekundu kwa wanaosoma tahasusi ya HGK. Pia aje na raba za kuchezea mpira wa miguu.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi (jozi mbili) vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi. Viatu aina ya jeje (mabuti) haviruhusiwi shuleni.

v. Soksi jozi mbili nyeupe/nyeusi/khaki za shule. vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.

vii. Sweta la rangi ya blue iliyokolea lenye shingo ya V. (inapatikana eneo karibu na shule kwa gharama ya tsh 15,000)

viii. Nguo za kushindia: Aje na suruali mbili za rangi ya dark blue, iwe na marinda mawili kulia na mawili kushoto isiwe yakubana yaani model, upana chini usipungue sentimeta 16. (inapatikana eneo karibu na shule kwa gharama ya tsh 20,000 kwa kila suruali)

ix. Awe na Tisheti (T-shirt) yenye kola na yenye nembo ya shule rangi ya njano aina ya form six. (Inapatikana eneo karibu na shule kwa gharama **tsh 12,000**).

x. Awe na truck suit ya rangi ya blue bahari iliyo kamili na koti lake. (Inapatikana eneo karibu na shule kwa gharama ya tsh 25,000)

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 7 aina ya counter book quire 3.

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (02) kwa mwaka.

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika anayosoma mwanafunzi.

iv. Scientific Calculator kwa wanafunzi wanasoma tahasusi ya **HGK**

v. Godoro la upana wa futi **2½** kwa futi **6.** (Yanapatikana eneo karibu na shule kwa gharama ya tsh 45,000)

vi. Mashuka Jozi mbili (light blue/blue isiyokolea), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.

**VIFAA VYA USAFI AMBAVYO WANAFUNZI WANAPASWA KUJA NAVYO**:

**1.TAHASUSI YA HKL**
Mwanafunzi aje na jembe na mpini wake,Kwanja,Fagio gumu (Hard bloom),Chelewa na sabuni ya maji ya lita tano (orginal)

**2.TAHASUSI YA HGK**
Mwanafunzi aje na jembe na mpini wake, brash ya mkononi,Dawa ya chooni aina ya Aro, brash ya chooni(hand brash) (Kishungi),panga, planka(zibulio)

xi. Sabuni ya kufulia, kuogea na Mafuta ya kupaka mwili.

**Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule namba **21801200077** Benki ya NMB jina la akaunti ni **SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA.**

Hatupokei fedha taslimu shuleni, risiti ya malipo yaani **pay slip ya bank (BPS)** iandikwe majina sahihi ya mwanafunzi. Ukifika shuleni hakikisha unaikabidhi kwa mhasibu wa shule kwa hatua zaidi.

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia

mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni pia mwanafunzi haruhusiwi kuwa na mavazi au alama zozote za kidini kwani shule hii sio ya seminari.

**MUHIMU:**

i. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

ii. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

iii. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
iv. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
vii. Uvutaji wa sigara;
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
ix. Kusababisha mimba;
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiii. Kudharau Bendera ya Taifa;
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;
xv. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
xvi. Kuvuka mto wami unaozunguka eneo la shule ambao una mamba na viboko.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule; Wenceslaus A.L. Kihongosi**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0754393921**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0656140560**
- **Mwandamizi Taaluma: 0763925630/0623830579**
- **Mwandamizi Malezi : 0789101171,**
- **Mwalimu wa Afya 0623227574**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**

**Bandika picha ya mwanafunzi hapa**

1. **TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

A. Jina kamili la mwanafunzi

i. JINA LA KWANZA……………………………………

ii. JINA LA BABA……………………………………….

iii. JINA LA UKOO……………………………………..

B. Tarehe yakuzaliwa………Mwezi………………Mwaka……………

**(Ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa)**

C. Mahali anapoishi mwanafunzi makazi yake ya kudumu;

Kijiji/Mtaa…………………………..Kata…………………

Wilaya……………………………………..Mkoa……………………

D. Mwanafunzi huyu ni YATIMA au SIYO YATIMA.( kama ni yatima eleza uyatima wake ni mzazi mmoja au wazazi wote)

…………………………………………………………………

E. Taarifa za shule ya Sekondari (kidato cha I hadi IV) uliyo Soma.

i. Jina la Shule ……………………………………………

ii. Namba yako ya mtihani kidato cha nne…………………

iii. Prem Namba ya mwanafunzi……………………………

***NB: kila mwanafunzi aje na nakala (copy) ya Result Slip na leaving certificate.***

F. Mawasiliano ya mwanafunzi.

i. Namba ya simu 1……………………………………Mzazi/Mlezi

ii. Namba ya simu 2……………………………………Mzazi/Mlezi

iii. Namba ya simu 3……………………………………Jirani

iv. Namba ya simu 4……………………………………Afisa Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa.

…………………………………………………………………

Jina, Saini na muhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa.

2. **TAARIFA YA MZAZI/MLEZI NA NDUGU WATAKAORUHUSIWA KUJA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI**

a) Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………

(Bandika picha yako kwenye kisandu juu)

b) Kazi ya mzazi/mlezi…………………………………………………..

c) Namba ya Kitambulisho cha Taifa ……………………………………

d) Anwani ya Mzazi/mlezi

S.L.P……………………..ENEO…………………..

e) Elimu ya Mzazi……………………………………………………………

f) Mtoto wangu ni MLEMAVU AU SIYO MLEMAVU (kama ni mlemavu taja aina ya Ulemavu wake).

…………………………………………………………………………………………

g) Ndugu ninao waruhusu kumtembelea mtoto wangu akiwa hapo shuleni ni.

i. Jina la ndugu: ……………………………………………………………

(Bandika picha yake kwenye kisandu juu)

ii. Uhusiano wake na mwanafunzi ………………..…………………..

iii. Mawasiliano yake: ………………………………………………………

i. Jina la ndugu: ……………………………………………………………

(Bandika picha yake kwenye kisandu juu)

ii. Uhusiano wake na mwanafunzi ………………..…………………..

iii. Mawasiliano yake:

……………………………………………………………

i. Jina la ndugu: ……………………………………………………

(Bandika picha yake kwenye kisandu juu)

ii. Uhusiano wake na mwanafunzi ………………..…………………..

iii. Mawasiliano yake:

……………………………………………………

**TAMKO RASMI LA KUSOMA NA KUELEWA TARATIBU ZOTE ZA SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA**

**1. MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………………………………………….

(taja majina yako yote matatu) wa kidato cha V tahsusi ya ……… Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa.

Ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule na kujifunza kwa bidii.

Sahihi……………………………………………... Tarehe……………………………..

**3. MZAZI/MLEZI:**

Nimehakikisha mwanangu ameisoma fomu ya kujinga na shule hii na nimemsisitiza katika kufuata sheria, taratibu na kanuni zote za shule, hivyo basi naamini mwanangu atakuwa mwanafunzi mtiifu muda wote awapo shuleni.

Maelezo mengine ya ziada toka kwa MZAZI/MLEZI ambayo ni muhimu Shule ikafahamu kuhusu mwanafunzi huyu.

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

Sahihi……………………………………………...

Tarehe…………………………….. …………

# KILOSA AGRICULTURAL SECONDARY SCHOOL

# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

***FROM:*** The Medical Officer,

………………………

P.O. BOX ……………..

………………………………….

***TO***: The Headmaster,

Kilosa Secondary School,

P. O. BOX 145,.

KILOSA **RE:**

**MEDICAL CERTIFICATE**

**(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

I have examined…………………………………… who seeks to join Form V in your school as follows:

| AREA | REMARKS |
|---|---|
| 1. Skin | ………………………. |
| 2. Eyes | ………………………… |
| 3. Ears | ………………………… |
| 4. Teeth | ………………………… |
| 5. Chest | ………………………… |
| 6. Spleen | ……………………….. |
| 7. Abdomen | ………………………… |
| 8. Urine | ………………………… |
| 9. Stool | ………………………… |
| 10. HB Hemoglobin | …………………………… |
| 11. Inoculation against meningitis | …………………………… |
| 12. Sickle cell | …………………………… |
| 13. Asthma | ……………………………. |
| 14. Any other comments | …………………………… |
| 15. blood Group | …………………………… |

Signature……………………………………

Date…………………………………………

Official stamp……………………………